

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**  
**IDARA YA UHAMIAJI**

ANUANI YA SIMU: "UHAMIAJI"  
TELEFAX: +255 26 2323532  
SIMU +255 26 2323542  
+255 26 2323543



OFISI YA KAMISHNA JENERALI WA  
UHAMIAJI  
4 BARABARA YA MWANGOSI,  
UZUNGUNI,  
S. L. P 1181,  
DODOMA.

28 Septemba, 2021

---

**TANGAZO LA AJIRA**

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji anatangaza nafasi za ajira 350 za cheo cha Konstebo wa Uhamiaji kwa vijana waliofuzu Mafunzo mbalimbali ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) waliopo Makambini au waliohitimu mafunzo hayo na wenye sifa zifuatazo:-

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 25.
- ii. Awe na Cheti cha Kuzaliwa (Birth Certificate),
- iii. Awe na Namba au Kitambulisho cha Taifa (NIDA).
- iv. Awe amehitimu Kidato cha Nne na ufaulu wa Daraja la Nne kwa Alama 28 hadi 31.
- v. Awe na Vyeti vya kuhitimu shule (Leaving Certificates),
- vi. Awe Vyeti vya taaluma (Academic Certificate),
- vii. Awe na Cheti cha Kuhitimu Mafunzo ya Awali ya JKT/JKU katika Oparesheni Mbalimbali.
- viii. Awe na afya njema ya mwili na akili, na aambatishe Taarifa ya Daktari kutoka katika Hospitali yoyote ya Serikali.
- ix. Awe na tabia njema, asiwe amewahi kufungwa, au kujihusisha na matumizi au biashara ya dawa za kulevya, au uhalifu wa aina yoyote.
- x. Asiwe na alama yoyote au michoro katika mwili wake.
- xi. Asiwe ameo au kuolewa.
- xii. Asiwe ameajiriwa/hajawahi kuajiriwa Serikalini.
- xiii. Awe tayari kuhudhuria Mafunzo ya awali ya Uhamiaji.
- xiv. Awe tayari kufanya kazi mahali popote nchini Tanzania.

**2. Waombaji watakaopewa Kipaumbele:**

Waombaji watakaopewa kipaumbele ni wale wenye taaluma ngazi ya Cheti kutoka katika Vyuo vinavyotambulika na serikali, wenye fani zifuatazo:-

Umeme, Ushonaji, Magari, Bomba, Uashi, Seremala, Taaluma za Uuguzi, Mtunza kumbukumbu za Ofisi, Katibu Muhtasi, Tabibu, Maabara, Udereva, Michezo, Muziki, Uimbaji, Sound Engineering, Mpiga Vyombo vya Muziki, Ugani pamoja na Fundi wa AC.

**3. Namna ya kufanya Maombi:**

Muombaji anatakiwa kuandika barua ya Maombi ya ajira kwa mkono wake akiambatisha nyaraka zifuatazo:-

- i. Barua ya Utambulisho toka Serikali ya Mtaa/Kijiji au Shehia,
- ii. Kwa waombaji waliopo Makambini, barua zao zipitie kwa Wakuu wa Kambi husika,
- iii. Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa,
- iv. Namba au Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Kitambulisho cha Mzanzibari,
- v. Vyeti vya kuhitimu shule (Leaving Certificates),
- vi. Vyeti vya Taaluma (Academic Certificates),
- vii. Vyeti vingine vya Fani mbalimbali,
- viii. Wasifu wa Mwombaji (CV),
- ix. Picha Nne (04) za Pasipoti zenye rangi ya Bluu.

**4. Maombi ya nafasi za ajira yanatakiwa yatumwe kupitia anuani zifuatazo:-**

- i. *Waombaji wenye Fani zifuatazo:- Mafundi wa Bomba, Seremala, Uuguzi, Tabibu, Mtaalam wa Maabara, Ugani na Fundi wa AC; wanatakiwa kuwasilishwa maombi yao kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji kupitia anuani ifuatayo:-*

NA	OFISI	ANUANI YA POSTA
1.	KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI, MAKAO MAKUU DODOMA	1181

- ii. *Kwa waombaji wa Fani nyinginezo wanatakiwa kuwasilisha maombi yao katika Ofisi za Uhamiaji Mkoa wanayoishi kupitia Afisa Uhamiaji Mkoa kwa anuani zifuatazo:-*

NA	AFISI UHAMIAJI MKOA	ANUANI YA POSTA
1.	ARUSHA	236
2.	DAR ES SALAAM	3315
3.	DODOMA	558
4.	GEITA	342
5.	IRINGA	404
6.	KAGERA	593
7.	KATAVI	68
8.	KIGOMA	190
9.	KILIMANJARO	1049
10.	LINDI	367
11.	MANYARA	398
12.	MARA	369
13.	MBEYA	791
14.	MOROGORO	994
15.	MTWARA	649
16.	MWANZA	1711
17.	NJOMBE	473

18.	PWANI	30109
19.	RUKWA	100
20.	RUVUMA	170
21.	SHINYANGA	426
22.	SIMIYU	454
23.	SINGIDA	360
24.	TABORA	292
25.	TANGA	371
26.	SONGWE	147

**iii. Waombaji wa Zanzibar wanatakiwa kuwasilisha Maombi yao kupitia Anuani zifuatazo:-**

NA	AFISI YA UHAMIAJI	ANUANI YA POSTA
1	KAMISHNA WA UHAMIAJI AFISI KUU YA UHAMIAJI ZANZIBAR	1354
2.	MJINI MAGHARIBI	1354
2.	KASKAZINI UNGUJA	1354
	KUSINI UNGUJA	1354
3.	KASKAZINI PEMBA	250
5.	KUSINI PEMBA (CHAKECHAKE)	195

**5. Mwisho wa kutuma Maombi ni tarehe 13 Oktoba, 2021.**

**6. Tahadhari;**

*Ikumbukwe kuwa Mwombaji yoyote atakayebainika kuwasilisha nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa Mahakamani.*

Limetolewa na,



SI - PAUL MSELLE  
**MSEMAJI MKUU WA UHAMIAJI**  
**MAKAO MAKUU - DODOMA**  
 28 Septemba, 2021